European Journal of
Linguistics
(EJL)

# Usawiri wa Wahusika wa Kiume katika Riwaya ya *Chozi La Heri*



CARI Journals

European Journal of Linguistics
ISSN: 2957-4641 (online)
Vol. 4, Issue No. 2, pp 41 - 48, 2025 www.carijournals.org

# Usawiri wa Wahusika wa Kiume katika Riwaya ya *Chozi La Heri*

**[1*]Agnes Mwongeli Kiema, [1]Dr. John Mutua, [2]Dr. Sarah Ndanu Ngesu**
[1]Machakos University
[2]South Eastern Kenya University.
https://orcid.org/0009-0007-9135-9121

*Accepted: 1st May, 2025, Received in Revised Form: 1st June, 2025, Published: 1st July, 2025*

**Ikisiri**

Makala hii imechunguza, usawiri wa wahusika wa kume katika riwaya ya *Chozi la Heri* (2017). Katika ulimwengu wa riwaya ya Kiswahili na fasihi, imekuwa kama jambo la kawaida kuona watafiti wengi wakichunguza masuala ya wanawake zaidi kuliko masuala ya wanaume. Jambo hili limetokana na ukweli kwamba, wanawake wamekuwa wakipiganiwa haki zao ili kuwafanya sawa na wanaume katika nyanja mbalimbali za maisha. Atieno (2019) anaeleza kuwa, kupuuzwa kwa jinsia ya kiume kumechangia hali yao ya upweke, kwani hakuna anayewafikiria wala kuwatetea kama inavyofanyiwa jinsia ya kike. Riwaya hii imeteuliwa kimakusudi kwa sababu inamsawiri mhusika wa kiume katika nyanja mbalimbali za maisha. Makala hii iliogozwa na nadharia ya uhalisia. Nadharia ya uhalisia inadai kwamba, fasihi inatakiwa kutoa picha halisi ya jamii husika. Nadharia hii ilizuka huko Ulaya katika karne ya kumi na tisa. Utafiti huu ulifanyika maktabani ambapo riwaya ya *Chozi la Heri* ilisomwa na kuhakikiwa. Ni matumaini yetu kuwa, Makala hii imetoa mwanga mkubwa kuhusiana na masuala ya jinsia ya kiume. Aidha, Makala hii itakuwa kichocheo cha watafiti wa baadaye wa fasihi kuchunguza masuala yanayohusu jinsia ya kiume.

**Maneno Muhimu:** *Usawiri, Wahusika, Uhalisia, Jinsia, Nadharia, Fasihi.*

European Journal of Linguistics
ISSN: 2957-4641 (online)
Vol. 4, Issue No. 2, pp 41 - 48, 2025 www.carijournals.org

**Utangulizi**

Mhusika ni kiumbe ambaye hupatikana katika kazi ya fasihi anayefanana na binadamu halisi kwa kiasi fulani. Kwa mujibu wa Mlacha (1985), wahusika ni watu ambao hubuniwa na msanii kutokana na maisha ya jamii yake na pia kulingana na anachotaka kukifahamu. Ili malengo ya mwandishi wa kazi ya fasihi yamfikie msomaji, kipengele cha wahusika lazima kitumike. Fasihi inahusiana na jamii naye mwandishi wa kazi ya fasihi ni zao la jamii. Hivyo basi, mwandishi wa kazi ya fasihi huandika mambo yanayohusiana na jamii, na hutumia wahusika kuwasilisha hali halisi ya maisha ya binadamu katika jamii fulani.

Katika jamii ya mtafiti kuna watu wa jinsia zote, yaani wanaume na wanawake na huo ndio uhalisia. Wanaume na wanawake hawa hujitokeza katika kazi ya fasihi kama wahusika. Kwa miaka mingi, jamii imekuwa ikimzungumzia mwanamke na kumsahau mwanamume. Isitoshe, masuala mengi yamechunguzwa kuhusu jinsia ya kike katika fasihi huku jinsia ya kiume ikisahaulika na masuala yao kutochunguzwa. Hivyo basi, ni wakati wa kuangalia upande wa jinsia ya kiume ambayo ilikuwa imepuuzwa kwa miaka mingi iliyopita, ili kuonyesha namna inavyosawiriwa katika kazi ya fasihi. Makala hii imechunguza usawiri wa wahusika wa kiume katika riwaya ya *Chozi la Heri*, kwa kuongozwa na nadharia ya uhalisia.

**Msingi wa nadharia**

Makala hii iliongozwa na nadharia ya uhalisia. Nadharia hii ilianza huko Ulaya katika karne ya kumi na tisa. Miongoni mwa wataalamu ambao walihusishwa na nadharia hii ni Georg Lukacs (1972) ambaye alikuwa mfuasi wa Marx. Nadharia hii inadai kwamba, fasihi inalenga kutoa picha halisi ya jamii husika. Tapo la uhalisia lilizuka kama vuguvugu la kuupinga mtazamo wa kilimbwende ambao ulishindwa kutatua matatizo ya wanajamii kwa sababu uliishia kwenye fikra za kijonzi. Tapo hili lilipingana na aina yoyote ya majaribio, hivyo basi mwandishi analazimika kuuteua mtazamo wa kisimulizi ambao utamwezesha kuyawasilisha maisha kwa "usahihi". Mulokozi (2017) anasema ya kwamba, fasihi iyasawiri maisha kama yalivyo bila kupotosha wala kutia chumvi huku ikijikita katika kuonyesha mahusiano na migongano ya kijamii, matatizo na pia matamanio ya mtu wa kawaida ndani ya jamii. Mwandishi wa riwaya ya *Chozi la Heri* amemchora mhusika wa kiume kama ambavyo mwanamume huonekana na kuchukuliwa katika jamii.

**Mbinu za utafiti**

Utafiti huu ulikuwa wa maktabani ambapo riwaya ya *Chozi la Heri* ilisomwa na kuhakikiwa. Aidha, maandishi yoyote yanayohusiana na mada ya utafiti huu yalisomwa ili kupata data ya kutosha kuhusiana na usawiri wa wahusika wa kiume. Fasihi andishi ina tanzu mbalimbali ambazo ni; riwaya, tamthilia, hadithi fupi na ushairi. Hata hivyo, utafiti huu ulichunguza usawiri wa wahusika wa kiume katika utanzu wa riwaya pekee. Hii ni kwa sababu, utanzu wa riwaya una mawanda mapana yanayoweza kutosheleza malengo ya utafiti huu. Uchambuzi huu ulihusisha riwaya ya *Chozi la Heri* (2017). Riwaya hii iliteuliwa kimakusudi kwa sababu inamsawiri mhusika wa kiume katika nyanja mbalimbali za maisha. Data iliyokusanywa ilichanganuliwa na kuwasilishwa kimaelezo.

European Journal of Linguistics
ISSN: 2957-4641 (online)
Vol. 4, Issue No. 2, pp 41 - 48, 2025 www.carijournals.org

**Matokeo ya utafiti**

Matokeo ya utafiti huu yalionyesha kwamba, mwandishi wa riwaya ya *Chozi la Heri* amemjadili mwanamume kama mhusika wa kihalisia katika masimulizi yake. Katika riwaya hii mhusika wa kiume amesawiriwa katika namna tofauti tofauti kama ifuatavyo.

**Mwanaume Aliyetelekezwa katika Jamii**

Mhusika wa kiume katika riwaya ya *Chozi la Heri* amepuuzwa na kutelekezwa. Hali hii inadhihirika kupitia kinywa cha Tetei ambapo mwandishi anasema kuwa, Jamii ya Wahafidhina inaipa kipaumbele pamoja na kuitetea jinsia ya kike, huku hukumu ya kifo ikipitishwa dhidi ya mwanamume, hata mume ambaye atapatikana na kosa la kumbaka mke wake. Inaelezwa kuwa, hata haki ya mtu kuhusiana kimapenzi na mkewe imebatilishwa na siasa hii ya usawa wa jinsia. Tunakubaliana na kauli ya Mohammed (2018) kuwa, wanawake wamekuwa wakipiganiwa haki zao ili kuwafanya sawa na wanaume katika nyanja mbalimbali. Jambo hili limesababisha kusahaulika kwa jinsia ya kiume katika jamii ya sasa. Msimamo wa mtafiti ni kwamba, mengi yachunguzwe kuhusu jinsia ya kiume hili kukiokoa kizazi kinachopotea nyikani, kwa kukosa matumaini ya kuishi.

**Mwanaume Aliyekosa Matumaini**

Mhusika wa kiume katika riwaya ya *Chozi la Heri* anaonekana kukosa matumaini katika maisha. Haya yanadhihirika ambapo baada ya familia ya Ridhaa kuangamia kwa moto naye kufukuzwa kwao, anaingiwa na huzuni na kukosa matumaini. Mwandishi anasema kuwa, baada ya kufukuzwa kutoka katika Msitu wa Heri, Ridhaa, Kaizari na familia yake waliishi katika Msitu wa Mamba kwa miezi sita. Baada ya kipindi hicho, walibahatika kurudi nyumbani kufuatia mradi ulioitwa na wanaharakati wa kupigania haki za kibinadamu: *Operesheni Rudi Edeni.* Hata hivyo, siku hii ya kurudishwa kwao ilikuwa siku ya hisia mseto kwa Ridhaa kwa kuwa hakuwa na familia ya kuendea, kwani wote isipokuwa Mwangeka walikuwa wamekwisha kuangamia.

**Mwanaume kama Kiumbe Asiye na Hisia**

Mhusika wa kiume katika riwaya ya *Chozi la Heri* anasawiriwa kama kiumbe asiye na hisia. Ridhaa anatatizika sana na milio ya kereng’ende na bundi usiku wa kuamkia siku ile ya kiyama. Kama anavyosema mwandishi, milio hii ilionekana kumtia Ridhaa kiwewe zaidi, kwani bundi hawakuwa wageni wa kikaida katika janibu hizi. Aidha, Ridhaa alijaribu kumjuza mkewe ila alipuuza na kumwambia kuwa, atakuja kujitia fadhaa bure kwa kujishughulisha na mambo ya ushirikina. Mazungumzo haya baina ya Ridhaa na mkewe Terry yalikuwa ya mwisho kabisa kutokea Terry akiwa hai.

Ridhaa anatamani kuwa angekuwa na muda zaidi wa kumuuliza mkewe maswali ambayo sasa yameivamia akili yake. Machozi yalifurika machoni, yakayaziba na kuulemaza uwezo wake wa kuona. Kama anavyoeleza mwandishi, Moyo wa Ridhaa ulipiga kidoko, ukataka kumwonya dhidi ya tabia hii ya kike ya kulia pindi mtu akabiliwapo na vizingiti ambavyo ni kawaida ya maisha, ukamakumbusha maneno ya marehemu mama yake siku za ujana wake. Mwandishi anaonyesha

mitazamo potovu waliyonayo watu kuhusu jinsia ya kiume. Msimamo wetu ni kwamba, iwapo makoo wanaruhusiwa kulia, basi hata majimbi wana hisia na wanapaswa kulia ili kuondoa uchungu na masikitiko.

**Mwanaume Aliyekosa Nafasi katika Jamii**

Katika riwaya ya *Chozi la Heri*, mhusika wa kiume amechorwa kama asiye na nafasi katika jamii ya Wahafidhina. Inaelezwa kuwa, vyombo vya habari na vikao vya wapigania haki vinapigania elimu ya mtoto wa kike, haja ya kuwainua akina mama kiuchumi huku hukumu ya kifo ikipitishwa dhidi ya mwanaume, hata mume ambaye atapatikana na kosa la kumbaka mke wake. Isitoshe, wahusika wa kiume katika riwaya ya *Chozi la Heri*, hawana nafasi ya kupitisha lolote hata katika vikao vya kitawala. Msimamo wa mtafiti ni kwamba, jinsia ya kiume na ya kike wapewe nafasi sawa katika jamii.

**Anayebaguliwa kwa Misingi ya Kiukoo**

Katika riwaya ya *Chozi la Heri,* Ridhaa anabaguliwa kwa sababu ametoka ukoo tofauti na watu wa ukoo wa Msitu wa Heri. Tunaelezwa kuwa, Ridhaa alitazamana ana kwa ana na tanuri la moto ambalo liliteketeza jumba lake la kifahari. Katika mkasa huu, familia yake iliangamia. Inaelezwa kuwa, Ridhaa hakuwa mkaazi asilia wa Msitu wa Heri. Alikuwa ‘Mfuata mvua’ kama walivyoitwa walowezi na wenyeji kindakindaki walionunua na kuhamia sehemu tofauti. Kama tunavyoarifiwa, baba yake Ridhaa alikuwa na wake kumi na wawili. Wake hawa walijaliwa na wana wa kiume ishirini na ndipo ardhi ya mzee Mwimo Msubili ikawa haitoshi kuwalea. Mzee Mwimo aliwahamishia wake wawili wa mwisho Msitu wa Heri. Mamake Ridhaa alikuwa mke wa mwisho wa Mzee Mwimo. Wakati huo, Ridhaa alikuwa mwenye umri wa miaka kumi na alikuwa bado hajaanza shule.

Walipowasili humu hamkuwa na wakaazi wengi na ilimchukua muda kuzoeana na watoto wa majirani ambao walimuona kama aliyekuja kuvuruga utulivu wao. Ridhaa alitengwa na wenzake siku ya kwanza shuleni katika michezo mbalimbali. Watoto hawa wamejifunza kutoka kwa wazazi wao kutoshirikiana na watu ambao si wa jamii zao. Isitoshe, katika riwaya ya Chozi la Heri wanajamii wana chuki na watu mbalimbali ambao wamehamia sehemu zao kwa njia ya kununua ile ardhi ambapo, watu hawa huonekana kama maadui kwa wanajamii asilia. Inaonekana kuwa, Ridhaa ameyafanya mengi mazuri kijijini hadi kikaacha kuitwa Kalahari. Hata hivyo, mke wa jirani anakuja kulalamika kuhusu kuuzwa kwa mashamba ya wenyeji kwa wageni, ambapo Ridhaa anagundua kuwa alikuwa mgeni wala si mwenyeji, hata baada ya kuishi pale miongo mitano. Halikadhalika, watu waliokula na kunywa pamoja naye, wanamlipulia aila na kusambaratisha maisha yake.

**Mwanaume kama Mvumilivu**

Katika riwaya ya *Chozi la Heri*, mhusika wa kiume ameonyeshwa kuwa ni mwenye uvumilivu. Hali hii inaonekana kupitia misukosuko mbalimbali ya kimaisha wanayopitia wahusika wa jinsia hii. Kwa mfano, tunamuona Ridhaa anavyokabiliwa na matatizo mengi na kuyavumilia. Mhusika

huyu anaonekana kuvumilia matukio yanayomkumba kijijini mwake, yakiwemo kutotakwa huko, mali yake kuharibiwa, familia yake kuangamizwa na kufukuzwa kwao. Halikadhalika Ridhaa anapofukuzwa kwao anaishi katika hali ya kudhalilisha kambini, anapoteza majumba yake katika mikasa tofauti tofauti. Hata hivyo, anaikubali hali hii. Uvumilivu unaonekana pia wakati Lunga anafutwa kazi katika shirika la Maghala ya Fanaka kwa sababu ya kupinga kitendo cha raia kuuziwa mahindi ya manjano kutoka ughaibuni. Mwandishi anaonyesha kuwa baada ya Lunga kuachishwa kazi, maisha yake yanabadilika na Naomi anakosa kuridhishwa na hali hii ambapo anaondoka na kumwachia watoto. Tunaona Lunga akivumilia maisha ya kuwa baba na mama wa watoto wake kwa muda kabla ya kifo chake. Hata hivyo wanayopitia wahusika wa kiume katika riwaya ya *chozi la heri*, wanayavumilia wakiamini kuwa maisha yatabadilika na kuwa mazuri. Kwa mujibu wa wafuasi wa nadharia ya uhalisia, fasihi ni kioo cha jamii. Hivyo basi inatakiwa kutoa picha halisi ya jamii. Ni kawaida kwa binadamu katika jamii halisi kukumbwa na matatizo na kuyavumilia akiamini kuwa, kuna njia zinazoweza kufanyika kusudi aweze kuyashinda. Ingawa mwanaume anakabiliana na changamoto nyingi katika maisha, anastahimili.

**Mwanaume Anayetumikishwa**

Utafiti huu umebaini kuwa, mhusika wa kiume katika riwaya ya *Chozi la Heri* anatumikishwa katika jamii. Aidha, mhusika wa kiume anadhalilishwa katika jamii ya Wahafidhina na nafasi yake haitambuliki. Inaelezwa kuwa, katika jamii ya wahafidhina kuna wakati ambapo wanaume walitumikishwa sana na wanawake waliokuwa mamlakani. Kupitia kinywa cha mhusika Tetei mwandishi anaeleza kuwa, katika enzi ya kisitimari wanaume walitumikishwa kutifua udongo mashambani, huku wanawake kama majeta wanakaa na kuwatumikisha. Hali hii inawafanya wanaume kuamini kuwa, mwanamke hapaswi kuongoza. Baada ya kutawazwa kwa kiongozi mwanamke, wanaume wanaonekana kushika silaha kupigania uhuru wao wakidai kuwa, watatumikishwa kama walivyofanywa enzi hizo. Wahusika wa kiume wanatoa kauli kuwa, mwanamke angewarudisha pale walikotoka. Aidha, wanalalamika kuwa, kwa miongo mitatu wanawake wamekuwa wakiwasumbua na *Affirmative action* na a *third should be a woman*.

**Mwanaume kama Mlezi Mwema**

Mwandishi wa riwaya cha *Chozi la Heri* amemchora mhusika mwanamume kama mlezi mwema. Kwanza, tunamuona Ridhaa licha ya shughuli za kikazi, akiwa nyumbani anatenga muda kucheza na wanawe na pia mjukuu wake Becky. Aidha, Mwangeka alikuwa akimwangukia baba yake akiigiza mpignaji masumbwi. Aidha, Ridhaa anaonekana kucheza na kijukuu chake Becky. Kinamwita babuu, naye Ridhaa anacheka. Halikadhalika, Ridhaa anaonekana kuwa mlezi mwema wakati anarudi nyumbani kutoka kazini na kuwapata watoto wake wakiigiza mazishi ya marehemu ndugu yao. Jambo hili linamkasirisha sana Ridhaa akahisi kama anasagwasagwa na wana aliowazaa. Inaonekana kuwa, baada ya kipigo cha babake Mwangeka aliapa kuwajibika zaidi, akainamia cha mvunguni katika masomo hadi chuo kikuu ambako alisomea uhandisi. Lunga naye anaonekana kuwa mlezi mwema anapoachwa na mkewe na kuachiwa watoto watatu kuwalea mpaka pale anapougua na kufariki**.** Inaonekana kuwa, anawalea watoto wake kwa njia nzuri huku

akiwahimiza kujiamini. Anawaonya dhidi ya kujishika tama. Riwaya hii inaakisi hali halisi ya jamii. Hii ni kwa sababu inamchora mhusika wa kiume kama jinsi ambavyo mwanamume huonekana katika jamii. Mwanamume katika jamii huwa na jukumu la kutunza na kulea familia yake kwa njia inayofaa. Ingawa mwanaume anaonekana kukabiliwa na changamoto nyingi maishani, anajitia nguvu na ktunza familia.

**Mwanaume Aliyelemewa na Ulevi**

Mwandishi wa riwaya hii amemchora mhusika wa kiume kama mlevi. Inaonekana kuwa, wanaume wasomi na ambao wamekosa nafasi za kazi waingilia matumizi mabaya ya vileo. Shamsi ambaye ana jina la msimbo Dengelua, anaishi katika mtaa wa Kazikeni ambao ni jirani wa mtaa wa Afueni anakoishi Ridhaa. Shamsi amesoma hadi Chuo Kikuu lakini amekosa nafasi ya kazi, jambo ambalo linamkatisha tamaa na kumpelekea kuingilia matumizi mabaya ya pombe, akawa mlevi wa kupindukia. Unywaji huu wa pombe wa kupindukia unamlazimisha mkewe kumwandama siku ya mshahara ili ajichukulie pesa za matumizi.

Shamsi ambaye anatembea kurudi nyumbani usiku wa manane akiwa amelewa chakari, anaimba wimbo ambao unasikika kama ngonjera. Wimbo huu ni wa kilevi.

Aidha, tunaona mwanafunzi wa uzamili anayenusurika kifo kutokana na kulewa pombe haramu. Inaelezwa kuwa, yeye na wenzake wanalewa ili kujisahaulisha changamoto wanazokabiliana nazo kama vile kutopata ruzuku au mikopo. Vijana hawa badala ya kutafuta mbinu nyingine za kujisaidia waingilia matumizi mabaya ya pombe haramu. Nadharia ya uhalisia mhimili usemao; fasihi inatakiwa kuonyesha picha halisi ya jamii, mwandishi wa riwaya hii anaakisi hali halisi ya jamii kwa kuwa, katika jamii wapo walevi ambao matendo yao yalingana na wahusika walevi katika riwaya hii. Maoni ya mtafiti ni kwamba, hatua ichukuliwe ili kuiokoa jinsia ya kiume inayopotelea ulevini kwa kukosa matumaini.

**Mwanaume kama Mwenye Msimamo Dhabiti**

Lunga ambaye ni mkurugenzi wa kitengo kinachoshughulikia uhifadhi wa nafaka katika Shirika la maghala ya Fanaka, anasimama imara kupiga kitendo cha raia kuuziwa mahindi amabayo yalikuwa yameagizwa kutoka ughaibuni. Mahindi hayo, licha ya kuwa na rangi ya njano yalihofiwa kuwa yameharibika. Huko ughaibuni yalikotolewa mahindi haya yalisemekana kuwa hatari kwa usalama hata wa panya. Tunaona kuwa, wataalamu wa masuala ya lishe walitia sahihi kuidhinisha uuzaji wa mahindi haya baada ya kushinikizwa na vigogo wenye shehena za mahindi haya. Inaelezwa kuwa, Lunga alikuwa na msimamao imara kulipiga tendo hili ili kuyaokoa maisha ya wanyonge wasio na hatia jambo ambalo lilimpelekea kupoteza kazi yake. wa kitengo cha Uhakikishaji wa Viwango na Ubora wa bidhaa.

Aidha Kang'ata anaonekana kuwa na msimamo imara kupiga ubaguzi wa kinasaba. Tunaona kuwa, anaridhia bintiye kuolewa katika ukoo ambao ni hasidi wa ukoo wake, jambo ambalo linajenga uhusiano bora kati ya koo hizi. Inaelezwa kuwa, Waombwe awali walikuwa maadui sugu wa ukoo Anyamvua. Hii ndio sababu ukoo mzima wa Anyamvua ulipiga ndoa ya Lucia kwa jino

na ukucha. Inaelezwa kuwa, ami zake Lucia walikuwa wamekataa katakata kuridhia ndoa yake. Kang'ata naye amabaye ndiye baba yake Lucia anaonekana kuwa na msimamo imara na kuridhia bintiye kuolewa katika ukoo ambao ni hasidi wa ukoo wake. Ni kawaida wanaume kuwa na msimamo dhabiti katika jamii wanapotaka jambo fulani kufanyika.

**Mwanaume kama Mtetezi wa Haki**

Shamsi ambaye ni mmoja kati ya wasimulizi wa hadithi ya *Chozi la Heri* anaonekana kuwa mtetezi wa haki. Yeye na wenzake wanalalamikia mishahara duni. Isitoshe, analalamikia kutwaliwa kwa shamba lao na kukosekana kwa dawa katika hospitali za wanyonge jambo linalosababisha kifo cha baba yake. Aidha, yule mja aliyekuwa amevaa shati lililoandikwa "Hitman" mgongoni anaonekana kuwa mtetezi wa haki. Huyu anaonekana kulalamikia ukosefu wa ajira, changamoto ambayo imeikumba nchi ya Wahafidhina. Katika jamii halisi, ni jambo la kawaida wanaume kuwa watetezi wa haki.

**Hitimisho**

Katika makala hii tulidhamiria kuchunguza usawiri wa wahusika wa kiume katika riwaya ya *Chozi la Heri,* kwa kuongozwa na nadharia ya uhalisia. Katika riwaya nyingi za Kiswahili, waandishi wamewasawiri wanaume kama viongozi wenye nguvu, ambao mara nyingi wanawadhulumu wanawake na kuwatawala katika jamii. Hata hivyo, riwaya ya *Chozi la Heri* inatoa mwelekeo mpya wa kiuandishi, ambapo wahusika wa kiume wanakutana na jamii iliyobadilika kiwakati, ambapo wao wenyewe wanadhulumiwa na kukadamizwa. Makala hii imebaini kuwa, mwandishi wa riwaya ya *Chozi la Heri* amemsawiri mhusika wa kiume kama, anayetelekezwa, aliyekosa matumaini, kiumbe asiye na hisia, anayebaguliwa kwa misingi ya kiukoo na kadhalika.

**Mapendekezo**

Utafiti huu ulichunguza usawiri wa wahusika wa kiume katika riwaya ya *Chozi la Heri.* Kwa kuwa hakuna utafiti unaoweza kukamilisha kila jambo, mtafiti anapendekeza yafuatayo kwa watafiti wa baadaye: Kwanza, utafiti ufanywe kuhusu usawiri wa wahusika wa kiume katika tanzu nyingine za fasihi andishi kama vile; ushairi, tamthilia na hadithi fupi. Halikadhalika, watafiti wa baadaye waweze kushughulikia suala la jinsia ya kiume katika tanzu za fasihi simulizi. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya uhalisia. Inapendekezwa kwamba, watafiti wengine wachunguze suala la jinsia ya kiume kwa kuongozwa na nadharia nyingine za uhakiki wa fasihi ili kutathmini matokeo ya utafiti.

**MAREJELEO**

Atieno, J. (2019). "Utambulisho wa jinsia katika *Maumbile si Huja* na *Paradiso*." Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Bayyo, F. (2020). "Usawiri wa jinsi ya kiume katika riwaya teule za Shafi Adam Shafi." Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Dodoma. (Haijachapishwa)

ISSN: 2957-4641 (online)

Vol. 4, Issue No. 2, pp 41 - 48, 2025


Lukacs, G. (1972). *Studies in European Realism*. The Universal Library GROSSET $DUNLAP, NEW YORK.

Matei, A. (2017). *Chozi la Heri*. Nairobi, Kenya.

Mlacha, S. (1985) "Wahusika katika riwaya ya Kiswahili (1970-1982)", Katika jarida la Mulika, Toleo la 17, Uk. 29-44, Dar es salaam, TUKI.

Mohammed, K. (2018). "Kuchunguza usawiri wa mhusika mwanamme katika riwaya ya Kiswahili: *Joka la mdimu* na Watoto wa *Mama N'tilie*. "Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu huria cha Tanzania. (Haijachapishwa)

Mulokozi, M. (2017). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*. Kauttu publishers.

©2025 by the Authors. This Article is an open access article distributed under the terms and conditions of the Creative Commons Attribution (CC BY) license (http://creativecommons.org/licenses/by/4.0/)